# MWANAHISA

CRDB BANK PLC www.crdbbank.co.tz


Disemba 2018 Toleo 12



CRDB BANK
The bank that listens

## Maoni kutoka kwa mwanahisa

Wanahisa wanapewa fursa ya kufikisha maoni, ujumbe au mapendekezo katika jarida hili kwa kutumia anuani ya mhariri.




# Vijue vipaumbele vya Mkurugenzi Mtendaji

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Bw. Abdulmajid Mussa Nsekela, amewahakikishia wateja, wanahisa na wadau wote wa Benki ya CRDB kuwa Benki hiyo ipo kwenye mikono salama na itaendelea kukua na kuzalisha faida.

Akielezea kuhusu vipaumbele vyake, Bw. Nsekela alisema kwa kushirikiana na viongozi na wafanyakazi wa Benki hiyo, amedhamiria kufanya maboresho makubwa katika utoaji huduma kwa wateja kwa kutilia mkazo maeneo matano muhimu ambayo ni; uboreshaji wa mifumo na taratibu za utoaji huduma ili ziendane na mahitaji halisi ya wateja na soko, kuongeza weledi na umahiri wa wafanyakazi, kuwekeza kwenye teknolojia ya kisasa, kukuza biashara katika nyanja zote ili kuendana na kasi ya Serikali ya awamu ya tano na kuhakikisha Benki inafanya vizuri na kupata faida zaidi ili kutoa gawio nono kwa wanahisa.

"Tutakuwa tukiboresha mara kwa mara taratibu za jinsi ya kupata na kutumia huduma zetu. Tunataka upatikanaji na utumiaji wa huduma za Benki yetu uwe rahisi, huku tukiendelea kusogeza huduma hizo karibu zaidi na wateja wetu" alisema Bw. Nsekela wakati wa mkutano na waandishi wa habari uliofanyika jijini Dar es Salaam. Mkutano huo ulikuwa na lengo la kumtambulisha rasmi Bw. Nsekela ambaye amechukua nafasi iliyoachwa wazi na Dkt. Charles Kimei ambaye amestaafu.

Akifafanua zaidi juu ya uboreshwaji wa huduma na mikakati ya Benki ya CRDB, Bw. Nsekela alisema kwa kipindi kifupi kijacho, Benki ya CRDB itajikita zaidi kwenye uwekezaji wa mifumo ya kidijitali itakayoiwezesha kuwafikia wateja wengi zaidi, kwa urahisi zaidi, mahali popote walipo na hivyo kuwaondolea wateja wao ulazima wa kutembelea matawi ya Benki ya CRDB pindi wanapohitaji huduma. "Kwa kuwa takwimu za mamlaka husika zinaonesha watanzania zaidi ya milioni 19 wanatumia simu za mikononi kufanya miamala yao, tutatumia fursa hiyo kuwashawishi kutumia bidhaa zetu za SimBanking na SimAccount ambazo nazo hutoa huduma kama hizo" alisema.

Bw. Nsekela alisema Benki ya CRDB imejiwekea malengo ya kufikisha huduma katika wilaya zote nchini ifikapo mwaka 2022 na kuongeza mawakala wa FahariHuduma katika kila kona ya nchi. Alisema Benki hiyo ina mpango wa kuendelea kupanua wigo wa huduma zake nje ya nchi.

Akielezea kuhusu mahusiano baina ya Benki hiyo na Serikali na wadau wengine, Bw. Nsekela alisema kuwa Benki ya CRDB inaitambua Serikali kupitia taasisi zake kama mwanahisa wake na mdau mkubwa wa biashara. "Benki ya CRDB itaendelea kuthamini mahusiano mazuri yaliyopo baina yake na Serikali na taasisi zake na kubuni huduma na bidhaa mbalimbali mahususi kwa ajili ya kufikia mahitaji ya Serikali na wafanyakazi wake. Tunajivunia kuwa miongoni mwa wadau wakubwa wa maendeleo na kwa kushirikiana na Serikali, tutaweza kujenga uchumi wa nchi hususani katika kipindi hiki ambacho serikali yetu inakusudia kujenga uchumi wa kati wa viwanda," alisema.

Bw. Nsekela alieleza kuwa hali ya uchumi nchini inatoa fursa kubwa kwa benki hapa nchini kuendelea kukua na Benki ya CRDB itatumia fursa hiyo kuboresha huduma kwa wateja wakubwa, wadogo na wa kati pamoja na biashara ya kilimo na kuwawezesha wawekezaji kwenye sekta ya viwanda.

Akizungumza katika Mkutano huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya CRDB Bw. Ally Hussein Laay alisema Bodi ina amini kuwa Bw. Nsekela ni mtu sahihi wa kuongoza Benki ya CRDB na kuahidi Bodi itampatia ushirikiano wa kutosha.

**Benki ya CRDB imejiwekea malengo ya kufikisha huduma katika wilaya zote nchini ifikapo mwaka 2022**

Bw. Laay alitumia nafasi hiyo kumshukuru Dkt. Kimei kwa mchango wake kwa kuiongoza Benki ya CRDB kwa mafanikio kwa kipindi cha miaka 20. "Ni kazi ngumu sana, lakini Dkt. Kimei ameifanya kwa kujitoa na weledi wa hali ya juu," alisema Bw. Laay.

# Benki yapata faida ya shilingi Bilioni 52 robo ya tatu Mwaka 2018

Benki ya CRDB na Kampuni zake Tanzu zimepata faida baada ya kodi ya shilingi bilioni 52 robo ya tatu Mwaka 2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia 79 kutoka faida ya shilingi bilioni 29 iliyopatikana robo ya pili mwaka husika. Benki na kampuni zake tanzu zimefanikiwa kupunguza wastani wa mikopo chechefu kutoka asilimia 13.1 (ya mikopo yote) robo ya pili mwaka 2018 hadi asilimia 8.96 robo ya tatu mwaka husika.

Kupungua kwa kiwango cha mikopo chechefu kulichangiwa na hatua kadhaa zilizochukuliwa na Benki ikiwemo kuundwa sera mahsusi ya kupunguza kiwango cha mikopo inayotolewa kwa kampuni kubwa na taasisi, na kujielekeza zaidi kutoa mikopo kwa wateja binafsi.

Jumla ya amana iliongezeka kutoka shilingi bilioni 4,425 robo ya pili mwaka 2018 hadi shilingi bilioni 4,511 robo ya tatu mwaka 2018. Jumla ya rasilimali za Kampuni za CRDB ilipungua kutoka shilingi bilioni 6,027 robo ya pili mwaka 2018 hadi shilingi bilioni 5,927 kipindi husika.

Pato kwenye mtaji liliongezeka kutoka asilimia 7.4 robo ya pili mwaka 2018 hadi asilimia 8.9 robo ya tatu mwaka 2018. Pato kwenye rasilimali liliongezeka kutoka asilimia 1.4 robo ya pili mwaka 2018 hadi asilimia 1.7 robo ya tatu ya mwaka husika.

Benki ya CRDB imeendelea kuongoza kwenye soko la huduma za kibenki kwa kuwa na kiwango kikubwa cha mizania na kushika asilimia 20 ya jumla ya amana na rasilimali katika sekta ya benki.

| Viashiria vya utendaji | Julai – Septemba 2018 (shilingi bilioni) | Aprili - Juni 2018 (Shilingi bilioni) | Kuongezeka/kupungua (kwa asilimia) |
|---|---|---|---|
| Rasilimali | 5,927 | 6,027 | 1.6 ▼ |
| Amana | 4,511 | 4,425 | 1.9 ▲ |
| Faida baada ya kodi | 52 | 29 | 79.3 ▲ |
| Mikopo iliyodorora | 8.96% | 13.1% | 4.14 ▼ |
| Pato kwenye rasilimali (ROA) | 1.7% | 1.4% | 0.3 ▲ |
| Pato kwenye Mtaji (ROE) | 8.9% | 7.4% | 1.5 ▲ |

# Wajue wajumbe wapya wa Bodi ya Benki ya CRDB.

Benki ya CRDB imepata wajumbe wawili wapya wa Bodi ya Wakurugenzi ambao wamepitishwa na Benki Kuu baada ya kuchaguliwa kwenye Mkutano Mkuu wa Wanahisa uliofanyika jijini Arusha Mei 19, 2018. Wajumbe hao ni Bw. Apollo Boniface Temu na Profesa Faustine Karrani Bee.

Bw. Temu na Prof. Bee wamechaguliwa kwa mara ya kwanza kuwa wajumbe wa Bodi kuwakilisha kundi la wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja. Katika uchaguzi huo, Bi. Rose Felix Metta alichaguliwa kuendelea kuwa Mjumbe wa Bodi kuwakilisha kundi la wanahisa wenye hisa kati ya asilimia1 na 10. Wajumbe hao wapya wanachukua nafasi za Bi. Devotha Ntuke Minzi na Bw. Juma Abdallah Abdulrahman ambao walijiuzulu baada ya muda wao kufikia ukomo.




Prof. Faustine Karrani Bee ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi -Moshi Cooperative University. Kabla ya hapo alikuwa Associate Professor-Chuo Kikuu cha Ushirika na Masomo ya Biashara-Moshi na mhadhiri kwenye chuo hicho. Prof. Bee ana Shahada ya Uzamivu katika masuala ya maendeleo kutoka Chuo Kikuu cha UNISA Pretoria, Shahada ya Uzamili ya masuala ya maendeleo kutoka Taasisi ya Masomo ya jamii –the Hague -Netherlands na Shahada ya Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.



Bw. Apollo Boniface Temu ni mtaalamu wa mambo ya Tehama. Baadhi ya nyadhifa alizowahi kushika ni; Naibu Mkurugenzi nchini -Path Digital Health Solutions, Mtendaji Mkuu wa Calderberg Group London, Kiongozi wa timu -Lloyds Banking Group London, Mtaalam Mwandamizi Ujenzi wa Miundo Mbinu -Distributed Business Service-Edinburgh na Mhandisi Mshauri masuala ya Tehama na Mkurugenzi Mtendaji -Calder System Limited. Bw. Temu ana Shahada ya Uzamili ya Sayansi (Information Technology Software Engineering) kutoka Chuo Kikuu cha Edinburgh Napier, Stashahada ya Juu na Stashahada ya Sayansi ya Kompyuta kutoka Institute of Management of Information System.

# Picha za matukio



Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa (kati) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya CRDB Bw. Ally Laay (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Bw. Abdulmajid Nsekela.






Spika wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Job Ndugai, Mkurugenzi wa Bodi ya Benki ya CRDB, Ndg. Ally Laay na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Ndg. Abdulmajid Musa Nsekela.

Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya CRDB Burundi, Ndg. Saugata Bandyopadhyay akiwa na Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Dkt. Charles Kimei wakiwa Burundi.






Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Ndugu Abdulmajid Mussa Nsekela akisalimiana na Waziri wa Fedha na Mipango nchini, Phillip Mpango.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Mussa Nsekela akisalimiana na Msajili wa Hazina, Ndugu Athuman Mbuttuka. Pembeni ni Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya CRDB, Ndugu Ally Hussein Laay

# Benki ya CRDB yang'ara tuzo za Soko la Hisa la Dar es Salaam




Benki ya CRDB imeendelea kung'ara baada ya kunyakua tuzo mbili za Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) zilizotolewa kutambua mchango na weledi wa taasisi wanachama.

Benki ya CRDB ilinyakua tuzo za Best Custodian na Main Investment Market (MIM). Tuzo hizo zilikabidhiwa kwa washindi na Msajili wa Hazina Bw. Athuman Mbuttuka ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye hafla ya utoaji wa tuzo hizo.

Akizungumza kwenye hafla maalum ya utoaji tuzo hizo, Mtendaji Mkuu wa Soko la Hisa la Dar es Salaam Bw. Moremi Marwa alisema kuwa lengo la tuzo hizo ni kutambua na kutunuku taasisi wanachama wa DSE kwa kufanya vizuri maeneo ya utawala bora, uwazi, mazingira, kulinda wawekezaji, ukuaji endelevu wa biashara na uwajibikaji kwa jamii.

Bw. Mbuttuka aliipongeza Benki ya CRDB na washindi wa tuzo nyingine na kusisitiza kuwa ofisi yake itaendelea kuwa karibu na wadau wake wote ili kuboresha utendaji katika sekta ya fedha.

## Mawasiliano

Mhariri
CRDB Bank Plc
Azikiwe Street
S. L. P. 268, Dar es Salaam, Tanzania
Simu Na. +255-22-211 2113
Fax na: +255-22-211 2113
Barua pepe: TullyEsther.Mwambapa@crdbbank.com

Katibu
CRDB Bank Plc
Office Accommodation Scheme
Mtaa wa Azikiwe, Ghorofa ya 4
S. L. P. 268, Dar-es-Salaam
Simu Na. 022 - 2114237, 2117442 - 7
Fax na. 022 - 2131005
Barua pepe: John.Rugambo@crdbbank.com au
shareholders@crdbbank.com
Au Meneja wa Tawi la Benki ya CRDB lililo karibu nawe